CRDB BANK

Tunakusikiliza

# NAFASI YA UJUMBE WA BODI

CRDB Bank Plc ni benki inayoongoza katika sekta ya biashara nchini Tanzania. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996, Benki imeendelea kukua na kustawi, na kujijengea nafasi kama mojawapo ya benki bunifu, imara na inayoaminika zaidi nchini. Hatua muhimu katika safari yake ilikuwa kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam tarehe 17 Juni 2009.

Kwa sasa, CRDB Bank Plc inamiliki kampuni tanzu nne; CRDB Bank Burundi S.A., CRDB Insurance Company Limited, CRDB Bank DR Congo S.A, CRDB Bank Foundation na Ofisi ya Uwakilishi iliyopo Umoja wa Falme za Kiarabu ( UAE-Dubai).

Bodi ya Wakurugenzi inakaribisha maombi kutoka kwa waombaji wenye sifa stahiki kwa nafasi moja (1) ya Mkurugenzi Huru na asiyehusika na utendaji wa kila siku wa Benki (Independent Non-Executive Director).

**“Mkurugenzi Huru” humaanisha mkurugenzi ambaye: (a) asiyekuwa na nafasi yoyote ya kiutendaji au ya usimamizi katika benki; (b) hana, moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, maslahi makubwa katika benki ikijumuisha benki mama au kampuni tanzu katika kundi moja; “Maslahi makubwa” humaanisha umiliki wa asilimia tano (5%) au zaidi ya hisa zenye haki ya kupiga kura; (c) hajaajiriwa na benki au kampuni zake tanzu katika nafasi ya kiutendaji kwa kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita; (d) si mwanafamilia wa mtu ambaye ni au aliyewahi kuwa mfanyakazi wa benki au kampuni zake tanzu katika nafasi ya kiutendaji ndani ya miaka mitatu iliyopita; (e) si mshauri wa kitaaluma wa benki au kampuni zake tanzu; (f) yuko huru dhidi ya mahusiano yoyote yanayoweza kuathiri uwezo wake wa kufanya maamuzi kwa uhuru; na (g) hapokei malipo yanayohusishwa moja kwa moja na utendaji wa benki kama inavyoelezwa katika Kanuni za Udhibiti wa Ndani na Ukaguzi wa Ndani, 2014.**

Jina la mgombea atakayekidhi sifa litawasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa ajili ya uteuzi. Tafadhali rejea Katiba ya CRDB Bank Plc (MEMARTS) kwa maelezo zaidi.

**Mahitaji ya Utaalam na Ujuzi**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(2) cha Kanuni za Utawala Bora za Benki na Taasisi za Fedha, 2021, mgombea anapaswa kuwa na utaalam na ujuzi katika mojawapo ya maeneo yafuatayo: Ubenki; Fedha; Uhasibu; Ukaguzi; Sheria; au Uchumi.

**Mahitaji ya Ujuzi**

Kwa kuzingatia mwenendo wa sasa wa soko, maendeleo ya kiteknolojia na ukuaji wa huduma za benki kidijitali, ujuzi ufuatao unahitajika: Muunganiko na Ununuzi wa Makampuni (Mergers & Acquisitions); Mifumo ya TEHAMA, Sayansi ya Data, Usalama Mtandao; Biashara ya Nje na Fedha za Miradi; Uhandisi; na Usimamizi wa Rasilimali Watu.

**Majukumu ya Bodi ya Wakurugenzi**

1. Kuweka dira, dhamira na maadili ya Benki ili kuhakikisha uendelevu na uwepo wa kisheria wa Benki.
2. Kufuatilia na kutathmini mikakati ya Benki ili kufanikisha dira na dhamira na kuhakikisha Benki inaendelea kustawi.
3. Kusimamia Benki kupitia sera na malengo ya jumla yaliyokubaliwa na Mkurugenzi Mkuu. Hii inajumuisha kuhakikisha kuwa:
   - Taratibu na mifumo ipo ya kulinda mali na hadhi ya Benki.
   - Benki inazingatia sheria, kanuni na viwango vya utendaji bora.
   - Teknolojia na mifumo inayotumika inatosheleza kuendesha shughuli za Benki kwa ufanisi.
4. Kufuatilia utambuzi wa hatari na usimamizi wake ili kuongeza thamani ya wanahisa.
5. Kuchagua na kuteua Mkurugenzi Mkuu ambaye atawajibika kusimamia shughuli za Benki na kutathmini utendaji wake mara kwa mara.

**Namna ya kutuma maombi**

Mwombaji anatakiwa kuwasilisha wasifu (CV), nakala zilizothibitishwa za vyeti vya kitaaluma, picha mbili za pasipoti, nakala ya ukurasa wa mwisho wa pasipoti, barua tatu za mapendekezo na tamko la madeni katika mabenki. Maombi lazima yapokelewe kabla ya saa **10:00 jioni Jumanne, 24 Februari 2026.**


Mawasiliano
**Katibu**
Makao Makuu CRDB Bank Plc
Kitalu Na. 25 na 26 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Kitalu Na. 21 Barabara ya Barack Obama
S.L.P 268, 11101 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 022-2219566
**Barua pepe: Boardmembers.Applications@crdbbank.co.tz**


**KWA IDHINI YA BODI**

Pascal T. Mihayo

**KATIBU WA BENKI**

17 Februari 2026